wa kutumia mbwa au silaha kali za moto kwa weledi.

Anasema: "Kutokana na

Matei anasisitiza: "Kampuni binafsi za ulinzi zina mchango mkubwa katika ulinzi na

nchi".

Mkurugenzi Mtendaji wa TT Security, Beatrice Eugen

katika maeneo mbalimbali nchini kutathmini changamoto na mafanikio ya kampuni hiyo

"Tathmini tuliyofanya mwaka 2023 kupitia kampuni

tukihimiza weledi mkubwa kwa kulinda watu na mali

ulinzi, TT Security imekuwa wakala mzuri wa kukusanya

Mwise.

Katika mazungumzo na

inatoa huduma za ulinzi kwa kutumia askari wasiovaa sare kutegemea mahitaji ya mteja.

* HABARI LEO UK 12.

# Pikipiki zachangia ubora mifugo, kilimo Mwanza



Mkuu wa Wilaya ya Misungwi, Paulo Chacha akimkabidhi pikipiki mmoja wa maofisa ugani mifugo, hivi karibuni Mwanza.

**Na Nashon Kennedy**

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu mkoani Mwanza, Fidellica Myovella ameshindwa kuficha hisia zake baada ya wataalamu wake sita wa Idara ya Mifugo kupatiwa pikipiki za kufanyia kazi kwa kusema binafsi amefurahi na kufarijika sana kwa tukio hilo.

Mkurugenzi huyo alitoa kauli hiyo katika mahojiano na gazeti hili hivi karibuni jijini Mwanza, wakati wa hafla ya ugawaji wa pikipiki kwa maofisa ugani kutoka wilaya zote za Mkoa wa Mwanza.

Myovela anasema kwa halmashauri yake kupatiwa pikipiki hizo sita zinaifanya iwe na jumla ya pikipiki 15 kati ya mahitaji ya pikipiki 39 kwa maofisa ugani wote wa halmashauri yake.

"Namshukuru kwa dhati ya moyo wangu kwa kutupatia pikipiki hizi ambazo zinakwenda kuongeza tija kwenye sekta ya mifugo," anasema na kuongeza kuwa yeye na watendaji wenzake watazisimamia vyema pikipiki hizo na kuhakikisha zinatumika kwa ajili ya malengo ya kusimamia ugani katika sekta ya mifugo.

Ofisa ugani wa Halmashauri ya Kwimba, Arsen Mwenda anasema amelemewa kwa furaha baada ya kukabidhiwa pikipiki ya kufanyia kazi.

Anasema pikipiki hiyo itamwezesha kutekeleza vyema majukumu yake kwa kutembelea kaya zote zenye mifugo kwa ajili ya kuangalia changamoto ambazo zinawakabili wananchi.

"Ilikuwa inaniwia vigumu kuwafikia wananchi hasa wafugaji. Naishukuru Serikali ya Rais Samia kwa kutupatia nyenzo hii. Siku za nyuma tulipata wakati mgumu kutimiza majukumu yetu," alisema Mwenda na kuahidi kuitunza vyema pikipiki hiyo.

Hiyo ni mara ya pili kwa Rais Samia Suluhu Hassan kununua pikipiki kwa ajili ya wataalamu wanaohudumia sekta ya mifugo na kilimo, ambapo mwaka jana alipatia Mkoa wa Mwanza jumla ya pikipiki 260 kwa maofisa ugani na kilimo kwa halmashauri zote za mkoa huo.

**KAULI YA SERIKALI**

Akizungumza kwenye hafla hiyo mara baada ya kukabidhi pikipiki 46 zilizonunuliwa na serikali na kugawiwa kwa maofisa ugani wa halmashauri zote nane za Mkoa wa Mwanza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa huo, Amos Makalla, Desemba mwaka jana, Mkuu wa Wilaya ya Misungwi, Paulo Chacha alisema lengo ni kuwawezesha maofisa hao kuchapa kazi ipasavyo.

"Zinakwenda kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao ya kutoa huduma za ugani kwa wafugaji na wakulima ili waweze kuzalisha kwa tija kuongeza pato lao na la taifa," alisema.

Chacha alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa namna anavyopambana kuimarisha sekta za mifugo na kilimo pamoja na ugawaji wa vitendea kazi kwa wataalamu.

"Tunamshukuru sana kwa msaada huu unakwenda kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma kwa wafugaji wetu na wakulima," alisema Chacha na kuwataka wataalamu waliokabidhiwa pikipiki wahakikishe kuwa wanavitunza na kuzitumia kwa malengo yaliyokusudiwa.

Aliwataka maofisa ugani hao kuhakikisha kuwa pikipiki hizo wanazitumia kwenye utekelezaji wa majukumu yao ya utendaji kazi kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma.

"Hizi pikipiki siyo muende kuzigeuza kuwa biashara ya bodaboda kwa ajili ya kujipatia kipato. Hapo mtakuwa mnakosea na hatua za kinidhamu zitachukuliwa, nendeni muwafuate wafugaji na wakulima walipo kwa ajili ya kutoa elimu ya kutosha kwao," aliwatahadharisha.



Maofisa ugani mifugo waliokabidhiwa pikipiki hivi karibuni mkoani Mwanza. (Picha zote na Nashon Kennedy).

Alisema kwa sasa katika Mkoa wa Mwanza hakutakuwepo kisingizio cha kwa nini wafugaji wasiwe na mifugo bora kwa uangalizi wa wataalamu kwa kufuata ushauri wao.

Alisema kwa miaka ya nyuma maofisa ugani kuna wakati walionekana kama wamesahaulika, mtu alikuwa akienda kwenye ofisi za maofisa ugani mifugo kupata huduma, lakini kutokana na uhaba wa vitendea kazi zilikuwepo changamoto nyingi.

"Lakini kwa kukabidhiwa pikipiki hizi, Serikali ya Awamu ya Sita imewapa heshima kubwa maofisa ugani mifugo hawa, wamepewa heshima na hadhi kama ofisa mwingine yeyote katika utumishi wa umma," alisema.

Katibu Tawala Msaidizi aliyemwakilisha Katibu Tawala wa Mkoa, Emil Kasagara alisema Mkoa wa Mwanza ulikuwa na jumla ya pikipiki nzima 41 na baada ya kupokea pikipiki hizo mpya 46 mkoa utakuwa na jumla ya pikipiki 87 na mahitaji ni pikipiki 150 na kuna upungufu wa pikipiki 55.

"Pikipiki hizo zimekuja wakati mwafaka kutokana na kuwepo na mradi wa kunenepesha ng'ombe na kituo atamizi kwenye shamba la taifa la mifugo Mabuki," alisema.

Naye Paulo Joseph, mkazi wa Nyakato jijini Mwanza anaishukuru serikali kwa kuwapatia maofisa ugani mifugo pikipiki hizo ambazo zitaongeza tija kwenye kusimamia uzalishaji wa mifugo na kilimo pia.

*Clarify na mwandishi juu ya cheo halisi cha maofisa hao waliokabidhiwa pikipiki. Je, ni Afisa Ugani au Afisa Ugani na Kilimo au Afisa Ugani-Mifugo?*

CamScanner